

## Maswali

1. Fumbo ni nini?
2. Mbona Yesu alifundisha watu akitumia fumbo?
3. Mtu wa kwanza alijenga nyumba yake kwa nini?
4. Mbona ilichukuwa mtu wa kwanza mda mrefu kujenga nyumba yake?
5. Mtu wa pili alijenga nyumba yake kwa nini?
6. Mbona mtu wa pili alichukuwa mda mfupi kujenga nyumba yake?
7. Nini ilifanyika usiku moja?
8. Nini ilifanyika kwa nyumba iliyojengwa kwenye mwamba?
9. Nini ilifanyika kwa nyumba iliyojengwa kwenye mchanga?
10. Yesu alifundisha nini kwa fumbo hii?

## Majibu

1. Fumbo ni hadithi ya somo.
2. Ni rahisi kukumbuka hadithi; hadithi inasaidia kukumbuka somo.
3. Mtu wa kwanza alijenga nyumba yake kwenye mwamba.
4. Ilichukuwa mda mrefu kujenga kwa sababu mwamba ulikuwa mgumu kujenga.
5. Mtu wa pili alijenga nyumba yake kwenye mchanga.
6. Alijenga nyumba yake kwa mda mfupi kwa sababu ilikuwa rahisi kuchimba kwa mchanga.
7. Usiku moja kulikuwa na dhoruba.
8. Nyumba iliyokuwa kwa mwamba ilisimama imara.
9. Nyumba iliyokuwa kwa mchanga ilianguka.
10. Tukijenga maisha yetu kwa Yesu, tutaishi vizuri. Mungu atatupa maisha ya milele. Tukijenga maisha yetu bila Mungu, hatutakuwa vizuri. Tutakufa milele na hatutaishi tena.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 31 Nyumba mbili

## Marejeo

Luka 6:47—49

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tunatakiwa tujenge maisha yetu kwa mafundisho ya Yesu. Lazima tufanye vile anataka.

## Maneno maalum

1. Mtu wa kwanza + ramani ya nyumba + msingi mzuri + mwamba.
2. Anza kujenga + kazi ngumu + malizia + nyumba nzuri.
3. Mtu wa pili + mvivu + haraka + rahisi + mchanga.
4. Dhoruba + upepo + mvua nyingi + mafuriko.
5. Nyumba ya kwanza + mvua ikanyesha + upepo ukavuma + simama imara.
6. Nyumba ya pili + mvua ikanyesha + upepo ukavuma + nyufa zikapasuka + nyumba ikaanguka.
7. Maisha yetu + zikiliza Yesu + tii + sahau Yesu maishani + tujifurahishe + kufa.



**31.1** Yesu aliambia watu hadithi nyingi. Hazikukuwa hadithi za kawaida. Tunaziita fumbo (mifano). Fumbo ni hadithi yenye somo. Yesu alifundisha watu akitumia fumbo kwa sababu ni raisi kukumbuka hadithi. Watu walipokumbuka hadithi, walikumbuka hata somo alilofundisha. Hii ni hadithi moja ya fumbo aliyofundisha juu ya watu wawili waliojenga nyumba- kila mtu yake.

**31.2** Kulikuwa na mtu aliyetaka kujengea familia yake nyumba. Alikuwa mtu wa akili na mwenye bidii. Alikaa chini na akachora ramani ya nyumba. Akafanya hesabu ya gharama. Akatembea akitafuta shamba ili ajenge nyumba. Alielewe ni lazima ajenge nyumba pahali pagumu na penye mwamba. Nyumba ilipaswa iwe na msingi imara. Aliendelea kuchunguza chunguza kwa mda mrefu. Baadaye alipata pahali pazuri. Alinunua hapo pahali. Akaanza kujenga nyumba. Ilikuwa ngumu kulima msingi kwa sababu ya mwamba. Huyu mtu alifanya kwa mda mrefu. Alijimba chini sana mwambani. Mwishowe alilainisha vile alitaka. Akawa tayari kujenga nyumba yake.

**31.2** Msingi ulipokuwa tayari, huyu mtu akaanza kujenga nyumba yake. Kila siku ukuta uliendelea kuja juu. Halafu akaweka paa. Mwishowe nyumba ikawa tayari. Familia yake ilifurahi sana. Wakahamia kwa hiyo nyumba mpya. Walifurahia sana makao mapya.

**31.3** Kulikuwa na mtu mwingine pia wa kujenga nyumba. Lakini huyu mtu alikuwa mvivu. Alitaka kujenga nyumba yake haraka sana. Hakutaka kufanya kazi. Hakutaka kujenga pahali pagumu penye mwamba. Hiyo itakuwa kazi ngumu, "nitajenga nyumba yangu kwa mchanga". Huyu mvivu alisema. "nirahisi kuchimba kwa mchanga." Huyu mvivu akachimba msingi haraka sana. Haikuchukuwa mda mrefu kuchimba pahali raisi pa mchanga mwepesi. Mara tu, nyumba yake ilimalizika. Familia yake ilifurahia. Walihamia kwa hiyo nyumba mpya. Walifurahia sana makao mapya.


**31.4** Siku moja kukatokea dhoruba. Upepo ukavuma na mvua ikanyesha sana. Mito zikafurika. Kukawa na gharika nchini.



**31.5** Upepo ulivuma na kupiga nyumba iliyokuwa kwa mwamba. Mvua pia ikanyeshea hiyo nyumba. Mito zikateremka kutoka vilimani. Maji yakapiga hiyo nyumba. Lakini ilikuwa imejengwa kwenye mwamba.

Nyumba ilisimama imara kwa mwamba. Upepo na mvua na maji haikutingiza hiyo nyumba. Nyumba ilikuwa ngumu sana. Nyumba ilisimama imara mwambani.

**31.6** Upepo ulivuma kwa nyumba ya mchanga. Mvua ikaipiga. Mito ikaosha na kuchukua mchanga chini ya nyumba. Hii nyumba haikujengwa kwa msingi wa nguvu. Nyufa zikaanza kuonekana. Maji yakapita ndani ya nyumba. Nyumba ikalegea. Upepo ukavuma na mvua ikanyesha. Mito ikaendelea kuchukuwa mchanga kutoka chini ya nyumba. Punde si punde kulikuwa na kishindo. Nyumba ya mchangani ikaanguka.



**31.7** Yesu alikuwa anafundisha somo kwa hii hadithi. Maisha yetu ni kama hizo nyumba. Tukijenga maisha yetu kwa mafundisho ya Yesu, tumpende na kumtii Mungu, maisha yetu yatakuwa na msingi bora. Tabia zetu zitakuwa nzuri. Mungu atatusaidia na kutuweka dhabiti katika ugumu wa maisha. Mungu atatupa maisha ya milele wakati Yesu atarudi hapa duniani. Tukijenga maisha yetu bila Mungu, tukiishi kujifurahisha sisi wenyewe, maisha yetu yatajengwa kwa msingi usio na nguvu. Tabia zetu hazitakuwa nzuri. Hatutafurahisha Mungu. Tukifa, hatutaishi tena. Kwa hivyo tumpende Mungu na tujenge tabia zetu nzuri kwa Mungu.